# UJUMBE WA WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI, MHE. NAPE M. NNAUYE (MB.) KATIKA MAADHIMISHO YA 43 YA UMOJA WA POSTA AFRIKA – (PAN AFRICAN POSTAL UNION (PAPU) TAREHE 18 JANUARI 2023)



NAPE M. NNAUYE (MB.)
WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

**Kauli Mbiu "Posta: Muwezeshaji anayekubalika na kutambulika kuendeleza biashara mtandao miongoni mwa nchi Afrika"**

Kwa kuadhimishwa mwanzoni mwa kila mwaka, Siku ya Posta Afrika inawapa wadau wa sekta ya Posta fursa ya kubadilishana salamu na ujumbe wa heri ya Mwaka Mpya.

Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ninaupongeza Umoja wa Posta Afrika (PAPU) kwenye maadhimisho haya ya miaka 43.

Tunapoangalia nyuma, tunakumbuka, kwa kujivuna na kutambua kwa heshima, namna mawaziri waliokuwa na dhamana ya mawasiliano Afrika walivyoona mbele na pia uamuzi wao tarehe 18 Januari 1980 mjini Arusha uliowezesha kuanzishwa kwa mojawapo ya taasisi zenye heshima kubwa Barani Afrika; yaani Umoja wa Posta Afrika (PAPU), ambao makao yake makuu yako kwenye ardhi ya Tanzania.

Kwa nchi nyingi za Afrika, miaka ya mwisho ya themanini na mwanzo wa tisini zimeshuhudia ~~ilishuhudia~~ mabadiliko ya kisera katika kusimamia uchumi, ikiwa ni pamoja na sekta za mawasiliano. Kipindi hicho pia kilichochea kwa kasi matumizi ya teknolojia ya habari na ~~ya~~ mawasiliano (TEHAMA), ambazo zilibadili mwelekeo na hatma ya sekta ya Posta katika nchi husika.

Simu za mkononi ziliongeza wigo wa habari na mawasiliano, na kusababisha idadi ya barua zilizopitia Posta za umma kushuka. Hilo lilitokana na simu za mkononi kuwezesha watumiaji kutuma ujumbe, nyaraka na data kupitia mtandao wa intaneti.

Hata hivyo, maendeleo haya yalileta fursa mpya kwa watoa huduma za Posta–hususan bBiashara mtandao ambayo imekuwa kipaumbele kwa nchi za Afrika-kama ilivyosisitizwa kwenye azimio la Afrika la mwaka 2020 kuhusu Kuibadili Afrika Kidijitali. Azimio hilo linataka kuwepo Soko Moja ya Kidijitali Afrika ifikapo mwaka 2030, ambapo hapatakuwa na mipaka ya watu, bidhaa, huduma na mitaji Barani humu.

Tanzania imetunga na kuweka mifumo ya kisera na kisheria inayolenga kuendeleza biashara mtandao nchini na nchi nyingine Afrika. Hii ni pamoja na kuendeleza uwekaji na uendeshaji wa miundombinu katika maneo yote yanayohusiana na biashara mtandao. Hili limefanyika kupitia utoaji wa leseni na uwekaji wa sera zinazochangia biashara mtandao; kama vile Sera ya TEHAMA ya 2016. Mengine ni kutunga Sheria ya Miamala Mtandaoni ya mwaka 2015 ambayo imeboreshwa mwaka 2022. Lengo ni kuimarisha usalama na imani; vitu ambavyo ni muhimu kwenye shughuli za biashara mtandao.

Pamoja na hilo, tunajivunia kuwa Tanzania imepiga hatua kwa kuondoa vikwazo vinavyokwamisha biashara mtandao, kuhakikisha miamala ya kielektroniki na taarifa binafsi za watumiaji ni salama.

Miaka tisa iliyopita, jijini Malabo, Equatorial Guinea, nchi za Afrika zilipitisha Mkataba wa Usalama Mtandaoni na Ulinzi wa Taarifa (data). Mkataba wa Malabo wa 2014 umeainisha mambo yanayofanikisha mifumo ya kisera na kiusimamizi kuhusu biashara mtandao, ikiwa ni pamoja na kuondoa vikwazo vinavyokwamisha kuenea kwake Afrika.

Chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali pia imeanzisha na inaimarisha mfumo wa kitaifa wa anwani za makazi, ambao unaongoza watoa huduma za Posta katika kufikisha bidhaa zilizonunuliwa kileketroniki. Mheshimiwa Rais ameonyesha azma ya ziada katika kuendeleza matumizi ya mfumo wa Taifa wa anwani za makazi. Kwa kuanzia, alihakikisha kuwa mfumo wa anwani umeingizwa katika utekelezaji wa Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika mwaka 2022. Pili, Rais alitembelea Ufalme wa Oman kushuhudia uwekaji saini wa makubaliano ya biashara mtandao kati ya Posta ya Oman na Shirika la Posta Tanzania.

Tanzania pia inatelekeza mpango wa kujenga mwelekeo tawala wa matumizi ya mifumo ya kidijitali katika uendeshaji uchumi, ukuaji huduma za jamii na utawala. Mpango wa Tanzania ya Kidijitali una vipengele vya kulibadili Shirika la Posta Tanzania. Lengo ni kuliwezesha shughuli zake kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia ili lishiriki kikamilifu kwenye biashara mtandao. Tanzania inataka kuwa kitovu cha biashara mtandao ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Mpango wa Tanzania ya Kidijitali pia unahusisha kufunguliwa vituo vya pamoja vya huduma mbalimbali za umma (vituo vya Huduma Pamoja) kwenye ofisi za Posta.

Tunapoadhimisha miaka 43 ya PAPU, Tanzania ina imani kuwa kubadilishana bidhaa na huduma miongoni mwa nchi za Afrika na kusambazwa na kufikishwa kwa bidhaa hizi kupitia mitandao ya Posta kutawezekana ndani ya kipindi kilichokusudiwa na Azimio la Umoja wa Afrika kuhusu Kuibadili Afrika Kidijitali (2020-2030).

Katika kuhitimisha ujumbe wangu, ninapenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyounga mkono wakati wote, ujenzi wa jengo la makao makuu ya PAPU jijini Arusha; ambalo litakapokamilika, na kuanza kutumika, litaongeza ufanisi wa Umoja huo katika kutoa huduma na pia litazalisha ajira zaidi kwa Watanzania.

Narudia kuupongeza Umoja wa Posta Afrika, nchi zote za Afrika, Wasimamizi wa sekta ya Posta, Watoa Huduma za Posta na Watumiaji wa huduma kwenye siku hii muhimu. Hongera Umoja wa POSTA Afrika kwa kuadhiminisha miaka 43 toka kuanzishwa.

Nape M. Nnauye (Mb.)
**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

# UJUMBE WA MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DK. JABIRI K. BAKARI KATIKA MAADHIMISHO YA MIAKA 43 YA PAN AFRICAN POSTAL UNION (PAPU DAY TAREHE 18 JANUARI 2023)

Leo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaungana na Jumuia ya Sekta ya Posta barani Afrika kuadhimisha miaka 43 ya Umoja wa Posta Afrika (PAPU). Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Sekta ya Posta barani Afrika na Sekretarieti ya PAPU yenye makao yake makuu jijini Arusha nchini Tanzania katika maadhimisho haya.

Kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu ni: **" "Posta: Mhamasishaji mahiri wa biashara mtandao ya kuvuka mipaka katika nchi za bara la Afrika").** Kaulimbiu hii inasisitiza jukumu linalofanywa na Sekta ya Posta la kuwa kichocheo kikuu cha kijamii na kiuchumi. Huduma za Posta zinatumia teknolojia kuboresha michakato ya biashara na kukidhi mahitaji ya wateja wenye ujuzi wa kidijitali - ili sekta hiyo iendelee kuwa na faida kibiashara katika soko shindani. Jukumu la Sekta ya Posta ulimwenguni kote ni kuwa kichocheo na pia daraja kati ya jamii katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi, vilevile kuwa na uhusiano wa karibu na sekta ya usafirishaji. Kuimarika kwa sekta ya usafirishaji kunahusishwa moja kwa moja na kuiwezesha Sekta ya Posta na biashara mtandao za kuvuka mipaka kati ya nchi na nchi.

Mahusiano thabiti ya biashara za kuvuka mpaka baina ya nchi jirani yamekuwa yakitekelezwa vizazi na vizazi, ila changamoto za biashara mipakani kati ya nchi jirani zilikuwa na bado zinatofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine. Vilevile, biashara za rejareja za kuvuka mipaka hasa zinazofanywa na jumuiya za nchi jirani kwenye vivuko maalum ya mpaka zimewezesha mtiririko wa uwekezaji wa mitaji kati ya nchi jirani unaoonekana kuimarika kutokana na uwazi mkubwa wa biashara na uwekezaji barani Afrika kama inavyowezeshwa na sekta ya Posta na Wabeba Virufushi na Vipeto (Couriers).

Biashara za mipakani, uwekezaji pamoja na uhamaji wa watu vilisababisha changamoto nyingi katika uchumi na jamii kwenye vipengele kama vile: sifa za kiuchumi, kisiasa, kijamii, miundombinu, mazingira na kitaasisi. Mwenendo wa biashara mtandao unaonyesha ongezeko kubwa la ubadilishanaji wa bidhaa mipakani ikilinganishwa na zamani, jambo lililothibitishwa na ustahimilivu wa Sekta hii ya Posta hasa wakati wa shida; kwa kuonyesha wazi mshikamano na hakikisho la kusaidia serikali na raia. Hii inaonesha Sekta ya Posta iko kati ya miundombinu muhimu sababu ya jukumu lake katika jamii wakati wote, kama vile ushahidi ulivyoonekana wakati wa majanga.

Sekta ya Posta imeshukudia hali ambayo haijawahi kushuhudiwa na hivyo mabadiliko ya mikakati ya kutoa huduma zetu kwa jamii ni muhimu katika kipindi hiki cha biashara mtandao. Ni wakati huu ambapo njia za kawaida za kuhudumia au kufanya biashara hazitumiki tena, wakati huu ni wa mabadiliko katika wigo wa utoaji wa huduma kulingana na mahitaji ya mteja kulingana na hali inayoendelea ya biashara isiyo na mipaka. Ushirikiano katika biashara mpakani unazidi hivyo jambo muhimu ni kuweka mazingira ya kuvutia ya biashara ya mipakani. Hivi karibuni Shirika la Posta la Tanzania na Shirika la Posta la Kenya walitia saini Mkataba wa kubadilishana Barua katika Vituo vya Mipakani na mipango kama hiyo inaendelea.

Biashara mtandao mipakani hukutana na changamoto hasa zinapoingia katika soko la kimataifa, katika mazingira ya mtandaoni, tofauti za tamaduni, sheria, kanuni, tabia, lugha, viwango vya teknolojia na aina tofauti za vibali. Vile vile, taratibu za kuvuka mipaka zinahusisha michakato mingi zaidi kuliko taratibu za ndani ya nchi, kama vile sheria na kanuni, teknolojia, malipo ya kuvuka mpaka, na kibali cha forodha ya kielektroniki.

Hata hivyo makampuni madogo, ya kati hadi mashirika makubwa ya kimataifa, sasa yanashughulikia changamoto za mahitaji ya mtandaoni yanayohusu wateja wa ndani na nje ya nchi. Nchi nyingi zilizoendelea na zinazoendelea zimekuwa zikitafuta mazingira ya uwazi na endelevu ya biashara mtandaoni ili kufikia uwezo kamili wa biashara ya kielektroniki ya kuvuka mipaka.

Biashara-mtandao huwezesha bidhaa kufikia wateja duniani kote wakati wowote wanapotaka kununua na kutoa urahisi wa kununua kwa mteja mwenye mahitaji mengi. Kwa sasa, biashara-mtandao ya kuvuka mipaka naendelea kuongezeka kwa kasi zaidi ikilinganishwa na biashara-mtandao ya ndani ya nchi; kwa maana hiyo unahitajika mkakati wa mgawanyo wa rasilimali ili kuongeza fursa mpya zinazosaidia kukuza soko na mauzo.

Ili kushughulikia changamoto za mahitaji na kuwezesha biashara za mipakani kukua, taasisi za fedha na mawakala wao wameanza kutafuta njia bora za kuwezesha biashara-mtandao; kwa kuanzisha malipo kupitia majukwaa mbalimbali kwa ajili ya mauzo ya bidhaa zinazoagizwa na kuuzwa mtandaoni ambapo kwa sasa wateja wanapendelea kuagiza mtandaoni na kuendelea kusubiri kuletewa mlangoni kupitia sekta ya Posta.

TCRA tayari imeanza kufanyia kazi mabadiliko yanayotarajiwa kwa kuandaa majukwaa kwa kushirikiana wadau wa Sekta ya Posta kupitia upya miongozo mbalimbali kwa kuweka upya viwango vya huduma za usafirishaji wa barua, vifurushi na vipeto; ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika biashara-mtandao mipakani. Tayari kuna majukwaa makubwa ya biashara-mtandao yanayofanya biashara nchini kama vile eBay & Amazon (Marekani), Ali Express (China), Jumia (Afrika) na Wildberries (Urusi) , pia wako wazalishaji na wasambazaji wa bidhaa mbalimbali wamejitokeza ili kujaza mapengo yanayojitokeza ya mnyororo wa usambazaji bidhaa na biashara mtandao ndani na nje ya nchi. Tofauti na biashara ya za zamani, biashara mtandao inahusishwa na utoaji wa bidhaa toka kwa nzalishaji hadi mwisho mnyororo mzima wa usambazaji; Lazima mnyororo wa usambazaji bidhaa na biashara mtandao ndani na nje ya nchi ipangiliwe ipasavyo kulingana na wakati tulio nao.

TCRA pia itaendelea kufuatilia kwa karibu utendaji kazi wa Sekta nzima ya Posta ili kuhakikisha ufanisi na ubora katika huduma zinazotolewa ili kutoa mchango chanya katika ufanisi wa biashara-mtandao.

Naomba nitumie nafasi hii kusema machache kuhusiana na udhibiti wa sekta ya Posta nchini. Hadi sasa TCRA imetoa leseni kwa Watoa Huduma 77 za Posta na Vifurushi katika makundi sita tofauti kama ifuatavyo:

| Na | Kundi la Leseni | Jumla |
|---|---|---|
| 1 | Mtoa Huduma za Posta wa Umma | 1 |
| 2 | Huduma za vifurushi na vipeto Kimataifa | 6 |
| 3 | Huduma za vifurushi na vipeto Afrika Mashariki | 1 |
| 4 | Huduma za vifurushi na vipeto ndani ya nchi | 26 |
| 5 | Huduma za vifurushi na vipeto Mji mmoja | 10 |
| 6 | Huduma za vifurushi na vipeto kati ya miji miwili | 33 |



**MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DK. JABIRI K. BAKARI**

TCRA iko tayari kushauriana na wadau wa Sekta ya Posta ili kuwezesha makampuni na watumiaji wa huduma za posta kufaidika zaidi na mabadiliko ya kiteknolojia, kijamii na kiuchumi yanayotokana na maendeleo ya ubadilishanaji wa bidhaa mpakani kupitia Sekta ya Posta.

TCRA imejizatiti kufanya kazi kwa Ushirikiano wa karibu na PAPU kwa ajili ya kutimiza dhamira yake, kadri inavyowezekana kwa manufaa ya pande zote. Tunaitaka PAPU kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha kuwa inajiimarisha Sekta ili iwekichocheo cha maendeleo ya kijamii na kiuchumi barani Afrika kwa kukuza biashara-mtandao mipakani ndani na nje ya Afrika.

Kwa niaba ya Bodi, menejiment na wafanyakazi wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, nawatakia wadau wote wa sekta hii ya posta heri mwaka mpya 2023. Vilevile napenda kuchukua fursa hii kuipongeza sekta ya posta ya Afrika na Sekretarieti ya Umoja wa Posta ya Pan African iliyoko Arusha katika maadhimisho haya ya miaka 43.